# Pata Matunzo ya Ebola Mapema



# Pata Matunzo ya Ebola Mapema





# Pata Matunzo ya Ebola Mapema




Ikiwa mupendwa wako ni mugonjwa na unafikili kuwa ana  Ebola, piga simu kwa kupata usaidizi. Usiwaguzee, usiguze damu yao ao maji ya miili yao (matapiko, mavi, mukoyo, jasho). Uwaambie wakunywe Muchanganyiko Solution de Réhydratation Orale (SRO) ao maji. Wagonjwa wanaokunywa SRO mingi mapema wana bahati ya ya kuishi. Usiguze kopo ile mugonjwa anatumia. Jaza kopo tena bila kuiguza. Nawa mikono yako mara mingi unapoongoja kupata usaidizi.

# Pata Matunzo ya Ebola Mapema








Ikiwa uko na mupendwa wako mugonjwa, ambulance ni njia nzuri sana kumufikisha pahali pa matunzo. Usitumie taxi ao magari mengine ya wasafiri. Ikiwa mupendwa wako atapelekwa mapema kwa pahali pa matunzo, anakuwa na bahati sana kupona kutoka Ebola. Hii inasaidia kuchunga jamaa yako.

# Pata Matunzo ya Ebola Mapema





# Pata Matunzo ya Ebola Mapema





Mupendwa wako atapokea utunzaji ya mapema iliyo bora zaidi katika pahali ya matunzo. Yeye atapokea SRO mingi  na madawa ya moto na alama zile zingine. Mufanyakazi wa afya katika pahali pa matunzo, aliye na mavazi ya kujichunga, anaweza kushurulikia mugonjwa muzuri zaidi kuliko ku mungini.





Mupendwa wako ana nafasi muzuri zaidi ya kupona kutoka Ebola ikiwa atapokea utunzaji ya mapema wa, mara moja tu alama zinapoonekana.